# *GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR*

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXIII Nam. 7242** **24 Aprili, 2024** **Bei, Shs. 3,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*


**YALIYOMO** *Ukurasa*


Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo. .................................. 236


**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Mswada**

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**TANGAZO**

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 15 Mei, 2024 kwa kusomwa mara ya kwanza, pili na tatu na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR** (Mhandisi Zena Ahmed Said)
24 Aprili 2024 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***


Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2024 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**2**. Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu zake husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UTARATIBU WA KODI, NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**4.** Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza neno jipya “asilimia” mwishoni mwa kifungu kidogo cha (2).

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**5.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**6.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza ufafanuzi wa maneno mapya katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

“mkaazi” maana yake ni mtu ambaye makaazi yake ya kudumu ni Zanzibar;

“huduma zilizoingizwa” maana yake ni huduma iliyotolewa kwa mlipakodi ikiwa usambazaji wa huduma umefanywa na mtu asiyekuwa mkaazi;

(b) kufuta ufafanuzi wa maneno "Mauzo yaliyosamehewa kodi" na "uingizaji" na kuweka badala yake maneno mapya katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"msamaha" kuhusiana na mauzo au uingizaji, maana yake ni mauzo au uingizaji ambao umeainishwa kama msamaha chini ya Sheria hii;

"uingizaji" maana yake ni kuleta au kusababisha bidhaa kuletwa Zanzibar kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(c) kufuta maneno "au huduma" katika ufafanuzi wa neno "Uhamishaji".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**7**. Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Kamishna anaweza kukasimu uwezo au utekelezaji wa jukumu lololote alilolopewa chini ya Sheria hii kuhusiana na usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya Ongezeko la Thamani katika huduma ya kielektroniki ya mlipakodi asiyekuwa mkaazi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba yake."

Kuongeza vifungu vipya vya 4A na 4B.

**8**. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 4A na 4B mara baada ya kifungu cha 4 kama ifuatavyo:

Mwakilishi wa mlipakodi asiyekuwa mkaazi.

**4A**.-(1) Mlipakodi asiyekuwa mkaazi anayefanya shughuli za kiuchumi Zanzibar bila ya kuwa na eneo maalumu ndani ya Zanzibar, na anafanya mauzo ambayo mlipakodi asiyekuwa mkaazi anawajibika kulipa kodi ya ongezeko la thamani:

(a) atateua mwakilishi wa kodi ya ongezeko la thamani Zanzibar kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa katika kanuni; na

(b) ikiwa itahitajika na Kamishna, ataweka dhamana.

(2) Mwakilishi wa kodi ya ongezeko la thamani atapaswa kuwa ni mkaazi na atawajibika kutekeleza mambo yote yanayohitajika kufanywa na Sheria hii, ikijumuisha:

(a) kuomba usajili au kusitisha usajili na kukamilisha masharti mengine yanayohusiana na usajili; na

(b) kulipa kodi ya ongezeko la thamani au faini, adhabu au riba yoyote iliyowekwa kwa mlipakodi asiye mkaazi chini ya Sheria hii.

(3) Usajili wa mwakilishi wa kodi ya ongezeko la thamani utakuwa katika jina la mlipakodi asiye mkaazi.

(4) Mwakilishi wa kodi ya ongezeko la thamani anaweza kumuwakilisha mlipakodi asiye mkaazi zaidi ya mmoja na mwakilishi huyo atajisajili katika kodi ya ongezeko la thamani kwa kila mlipakodi asiye mkaazi anayewakilishwa.

Huduma kutoka tawi la nje ya Zanzibar.

**4B**.-(1) Endapo mlipakodi anafanya shughuli za kiuchumi ndani ya eneo maalumu Zanzibar na katika eneo moja au zaidi maalum nje ya Zanzibar:

(a) mtu huyo atachukuliwa kama watu wawili tofauti kulingana na shughuli za kiuchumi zinazofanyika ndani na nje ya Zanzibar;

(b) mtu ambaye yuko nje ya Zanzibar atachukuliwa kuwa anafanya mauzo ya uingizaji wa huduma kwa mtu aliye ndani ya Zanzibar ikijumuisha faida yoyote kutokana na huduma husika aliyepatiwa mtu huyo ndani ya Zanzibar kupitia au kama ni matokeo ya shughuli iliyofanywa na mtu nje ya Zanzibar; na

(c) muda wa mauzo utatambuliwa kwa kukisia kuwa mauzo yamefanyika.

(2) Endapo, ndani ya miezi kumi na mbili kutoka tarehe ya kufanya mauzo iliyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu aliye nje ya Zanzibar ataainisha mgawanyo wa gharama kwa mtu aliye ndani ya Zanzibar kuhusiana na mauzo, mgawanyo wa gharama itachukuliwa kama ni thamani ya mauzo.

(3) Endapo mauzo yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ni mauzo ya kodi, thamani ya mauzo:

(a) endapo masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki yatatumika, yatakuwa sawa na kiwango cha gharama kilichotengwa, kilichopunguzwa na sehemu hiyo, kama kipo, kwa kiwango kilichotengwa ambacho kinawakilisha:

(i) mshahara au malipo ya muda anayolipwa muajiriwa wa mtu aliye nje ya Zanzibar; na

(ii) riba inayoingiwa na mtu aliye nje ya Zanzibar; na

(b) katika mazingira mengine yoyote, itachukuliwa kuwa imefanywa na mtu asiye mkaazi nje ya Zanzibar ambaye anahusiana na mtu aliyeko ndani ya Zanzibar."

**9**. Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza maneno "bima, kidijitali," baina ya maneno "benki" na "posta". Marekebisho ya kifungu cha 8.

**10**. Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "au uingizaji" baada ya kila neno "mauzo" popote linapojitokeza katika kifungu. Marekebisho ya kifungu cha 10.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA, NAM. 8 YA 2017

**11**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**12**. Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya kifungu cha 9.

(a) kuongeza vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Mkuu wa Forodha, kwa madhumuni ya kudhibiti uingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa, ataweka stempu bidhaa zote zinazotozwa ushuru wa bidhaa wakati wa uingizaji kwa mujibu wa sheria inayosimamia uwekaji wa stempu ya bidhaa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "stempu" maana yake ni stempu ya kodi ya kielektroniki."; na

(b) kukipa namba upya kifungu kidogo cha (2) kuwa kifungu kidogo cha (4).

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA MAJENGO, NAM. 14 YA 2008

**13**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Majengo Nam. 14 ya 2008 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**14**. Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "siku ya thelathini ya Septemba ya kila mwaka, na kodi iliyolipwa itamaliza muda wake tarehe thelathini Juni kufuatia mwaka ambao kodi ilipaswa kulipwa" na kuweka badala yake maneno "siku ya thelathini na moja ya Disemba ya kila mwaka". Marekebisho ya kifungu cha 10.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI, NAM. 8 YA 2006

Kusomwa.

**15**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 8 ya 2006 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**16**. Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta maneno "Sheria ya Kodi ya Mapato" yanayojitokeza mwisho wa kifungu kidogo na kuweka badala yake maneno "Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Nam. 10 ya 2015".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**17**. Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuingiza maneno "au Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Nam. 10 ya 2015" mwisho wa kifungu kidogo.

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**18**. Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuingiza maneno "Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Nam. 10 ya 2015 na" mara baada ya maneno "masharti ya".

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kuweka na kurekebisha baadhi ya kodi na ushuru, na kufanya marekebisho ya sheria za fedha na kodi zinazohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hizo.

Kodi na ushuru uliowekwa zinakusudiwa kukusanywa na mamlaka za kodi na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kama mapato ya Serikali. Marekebisho ya sheria za kodi yanakusudia kurahisisha taratibu za ukusanyaji wa kodi, kuzifanya sheria za kodi ziendane na wakati kwa mujibu wa hali ya sasa na kuongeza mapato ya Serikali bila ya kuathiri maslahi ya umma.

Mswada huu umegawika katika Sehemu Sita:

***Sehemu ya Kwanza*** inajumuisha masharti ya awali ambayo ni jina fupi na kuanza kutumika.

***Sehemu ya Pili*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 katika kifungu cha 33 kwa kuingiza maneno "asilimia" mwisho wa kifungu kidogo cha (2) kwa ajili ya ufasaha.

***Sehemu ya Tatu*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998 katika kifungu cha 2, 3 na kuongeza vifungu vipya vya 4A na 4B. Aidha, sehemu hii imefanya marekebisho katika kifungu cha 8 na 10, ambayo yameanzisha dhana ya mlipakodi asiyekuwa mkaazi wa Zanzibar na taratibu za kuwadhibiti.

***Sehemu ya Nne*** inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017 katika kifungu cha 9, kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kwa kuweka taratibu za uwekaji wa stempu katika bidhaa zinapoingizwa Zanzibar.

***Sehemu ya Tano*** inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008 katika kifungu cha 10 kwa kufuta baadhi ya maneno na kuweka badala yake na maneno mengine kwa ajili ya ufasaha.

***Sehemu ya Sita*** inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 11 ya 2007 katika kifungu cha 29, 30 na 31 kwa ajili ya kuendana na mabadiliko yaliyofanywa katika Sheria.

ZANZIBAR
24 Aprili, 2024

**(Dkt. Saada Mkuya Salum)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR - 2024